JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.

SHULE YA SEKONDARI LWANGWA,

S.L.P 131

TUKUYU

……../……../2021

KUMB.NA.LWS/JO/VOL.1/04

Mkuu wa shule: 0752226682/0718927522
Makamu Mkuu wa Shule: 0765883535
Matron/ patron: 0765521643/0742336720
Mhasibu 0762016908

Mzazi/mlezi wa Mwanafunzi

……

S.L.P ……

……

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI LWANGWA.

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano Tahasusi (combination)……. katika shule hii mwaka wa masomo 2021/2022 .Shule itafunguliwa tarehe 05/07/2021. Mwisho wa kuripoti itategemea tarehe itakayotangazwa na Wizara.

MAHALI SHULE ILIPO.

Lwangwa sekondari ni shule ya serikali, shule hii ni ya kutwa kwa kidato cha I-IV na bweni kwa kidato cha V-VI iko Mkoani Mbeya, Wilaya ya Rungwe Halmashauri ya wilaya ya Busokelo umbali wa kilometa 41 kutoka Tukuyu mjini.

NAMNA YA KUFIKA SHULENI.

Unaweza kufika shuleni kwa kutumia usafiri wa namna mbili kama ifuatavyo:-

(i) Unaweza ukatumia basi linaitwa **SIKUTEGEMEA.** Basi hili linaanza safari yake **Lwangwa** kuelekea **Mbeya** jijini ambako linafika saa **3:00** asubuhi. Saa **3:30** asubahi linakuwapo eneo la Nanenane jijini Mbeya kwa ajili ya kuanza safari ya kurudi Lwangwa. Baada ya saa nne linaondoka jijini Mbeya. Basi hilo ni zuri kwa sababu ni usafiri wa moja kwa moja hadi shuleni pia linafanya kazi Jumatatu hadi Jumamosi . Jumapili halifanyi kazi.Ukilikosa basi hilo unaweza ukapanda basi aina ya **COSTA** kutoka jijini Mbeya hadi Tukuyu mjini ambako ukifika ulizia stand ya Lwangwa huko utayakuta magari ya kuelekea Lwangwa.Nauli ya kutoka Mbeya mpaka Lwangwa kwa basi hilo ni Tshs 6000/=na kutoka Mbeya mpaka Tukuyu ni Tsh3000/= na kutoka Tukuyu mpaka Lwangwa ni Tshs 5000/= kwa gari aina ya Noah.

MAAGIZO:

2:1. SARE NA VIFAA VINGINE.

1. Suruali/ sketi tatu (1)moja ya rangi ya dark bluu kitambaa cha istem namba moja.
   (2)Ya pili rangi ya gold kitambaa cha istem namba moja.
   (3) Ya tatu rangi ya kijivu kitambaa cha istem namba moja.
   Mwanafunzi ashone sare zote akiwa nyumbani zenye" turn" up na zisizo za kubana kipimo chini ni inch 16 (kwa wavulana) na sketi ndefu ziwe na malinda ya kawaida zinazoishia kwenye kifundo cha mguu (kwa wasichana).***lazima rangi ya gold na kijivu uje ushonee huku ili kuepusha kuchanganya vitambaa. Sweta la kijani lazima uje ununuee huku kuepusha kuchanganya rangi.***
2. Mashati meupe mawili ya mikono mirefu.
3. Viatu vyeusi vya kamba visivyo vya kisigino kirefu.
4. Soksi nyeusi ndefu kwa wavulana na nyeupe ndefu kwa wasichana .
5. Sweta ya rangi ya kijani jeshi lenye shingo ya umbo la V(Kuepusha kuchanganya rangi tunashaauri aje anunue huhuku)
   NB:Tunashauri aje anunue hukuhuku ili asichanganye rangi.
6. Aje na jaketi jeusi (sio koti ambalo litatumika wakati wa baridi kali).
7. Alete kwanja 1 lililonolewa, jembe 1 na mopa 1 au brashi 1 ndefu ya kufanyia usafi.
8. Alete ndoo moja kubwa ya plastiki kwa ajili ya matumizi ya shule na Ndoo ndogo 1 ya matumizi binafsi.
9. Aje na godoro 2 ½ x 6 pia yaweza kupatikana lwangwa madukani.
10. Aje na shuka jozi mbili rangi ya pinki na bluu bahari.
11. Aje na blanketi zito la kutosha kujisitiri kipindi cha baridi sana.
12. Aje na mto mkubwa pamoja na foronya mbili.
13. Aje na chandarua 1 ili kujikinga na mbu.
14. Aje na taulo 1
15. Aje na mswaki, dawa ya meno, sabuni za kutosha na kandambili.
16. Aje na sahani, bakuli na kikombe kwa ajili ya chakula {chakula kinatolewa shuleni}
17. Aje na Reki moja kwa wasichana kwa wavulana aje na panga.

NB***: Anapokuja kuripoti mwanafunzi awe amevaa sare za shule na haruhusiwi kuja na nguo nyingine ambazo hazitambuliwi na shule.Pia mwanafunzi asishone suruali inayobana ("modo) au sketi fupi adhabu kali itachukuliwa kwa mwanafunzi atakayekiuka agizo hilo.***

2:2 VIFAA VYA MICHEZO.

a) Bukta na fulana rangi ya blue kwa ajili ya michezo.
b) Soksi jozi moja ziwe ndefu.
c) Track suit rangi ya Blue
d) T-shirt yenye nembo ya shule (itapatikana shuleni kwa Tsh10,000/=fedha hiyo uje nayo mkononi.)
e) Raba za michezo kwa wote.

2:3. VIFAA VYA MASOMO:

Unatakiwa kuleta vifaa vya masomo kama ifuatavyo:-

Madaftari makubwa (caunter book) kwa masomo yote saba utakayosoma.

- Scientific Calculator fx 991 (kwa wanafunzi wa sayansi)
- Kalamu za wino (bluu na nyeusi) na risasi.
- Mkebe wa Hisabati (mathematical set)
- Four figure table/ mathematical table.

- ❖ Ni muhimu kwa kila mwanafunzi kuja na vitabu vya masomo atakayosoma.
- ❖ Ream moja.A4 kwa mwaka (iletwe shuleni)
- ❖ Aje na kamusi ya Kiswahili na kiingereza (Oxford Advanced Learners Dictionary)kwa mwanafunzi wa mchepuo wa HGL,HGE na HGK. **Kamusi ya Kiswahili**

2:4. <u>FEDHA</u>

i. Ada ya shule kwa wanafunzi wa bweni ni shs.70, 000/= kwa mwaka, yaani .Sh. 35,000/= kwa kila muhula.
ii. Fedha ya tahadhari Sh.5,000/=
iii. Kitambulisho na picha Sh.6,000/=
iv. Taaluma Shs:20,000/=kwa mwaka
v. Ukarabati sh. 30,000/=
vi. Tsh: 30,000/= kwa mwaka watumishi wasio walimu
vii. Aje na fedha za kutosha kwa ajili ya matibabu ambapo atajigharimia mwenyewe,au aje na Bima ya afya ya Taifa NHIF,au aje na Tshs 6,000/=kwa ajili ya kukatiwa Bima ya Afya (CHF) iliyoboreshwa.
viii. Umeme kwa mwaka Tshs 15,000/=kwa mwaka
NB. JUMLA YA MICHANGO YOTE KWA MWAKA NI Tsh. 176,000/=. Inalipwa kwa awamu mbili, awamu ya kwanza ni julai2021 TSH. 108,500/= awamu ya pili ni januari2022. TSH. 67,500/=.

Fedha zote zilipwe benki kwenye A**/C N0. 61403500101 NMB (Lwangwa Sec School revenue collection account)** original pay in slip ziwasilishwe shuleni **isipokuwa fedha ya T-shirt TSHS10,000/=italipwa shuleni na fedha TSHS 6,000/=kwa ajili ya CHF ambayo atakatia hiyo bima hukuhuku.Fedha hizo zisiwekwe kwenye akaunti ya shule aje nazo atakapokuwa anaripoti.**

2:5. <u>KABLA YA KUJA SHULENI VEMA KUTIMIZA YAFUATAYO:-</u>

i. Kupimwa na daktari wa Hospitali ya serikali. Tumia fomu iliyoambatanishwa.
ii. Kuleta cheti cha kuzaliwa (nakala) au “affidavit” ambayo hupatikana mahakama ya Wilaya.
iii. Kusoma na kuzielewa sheria/ kanuni za shule (zimeambatanishwa)
iv. Kujaza fomu ya taarifa binafsi iliyoambatanishwa.
v. Kuhakikisha kuwa unakuja na **result slip** kwa ajili ya kusajiliwa bila hivyo hutapokelewa wala kusajiliwa.
vi. Hakikisha malipo yote yamefanyika kikamilifu.
vii. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na **simu** shuleni.

2:6.<u>SHERIA NA KANUNI ZA SHULE</u>.

Kila mwanafunzi atatakiwa kufuata na kutekeleza sheria na kanuni zote za shule kama inavyotakiwa.(zimeambatanishwa)

Hongera kwa kubahatika kupata nafasi hii ya pekee kati ya maelfu ya wanafunzi waliofanya mtihani. Hivyo ni lazima kuitumia nafasi hii vizuri kwa faida yako na Taifa. Kinachokuleta katika shule hii ni kujifunza na kuelimika.Hivyo unatakiwa kudumisha heshima na sifa ya Shule hii ya **LWANGWA.**

Unapofika ripoti kwa Mkuu wa shule au Makamu mkuu wa shule hii ili upewe maelekezo.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Saini ya Mkuu wa shule……

Jina la Mkuu wa shule: SIMON G.NJEJE

Mhuri wa Mkuu wa shule……

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.
SHULE YA SEKONDARI YA LWANGWA
SHERIA NA KANUNI ZA SHULE YA SEKONDARI LWANGWA

Shule ya sekondari Lwangwa inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu ya **Na-25** ya mwaka **1978.** Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

Wewe kama mwanafunzi unapaswa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

a) Kuheshimu viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii inayotuzunguka.
b) Kuhudhuria vipindi vyote vya darasani pia shughuli zote za ndani na nje ya shule.
c) Kuwahi shuleni asubuhi na kutekeleza shughuli zinazopaswa kabla ya vipindi.
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu juu ya kuwepo ndani au nje ya mipaka hiyo.
e) Kutunza usafi binafsi na mazingira ya shule kwa ujumla.
f) Kuvaa sare ya shule uwapo ndani ya shule na unapotoka nje ya shule.
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, ni pamoja na maandalio ya jioni (preparation).
h) Huruhusiwi kumiliki au kutumia simu uwapo shuleni pasipo idhini maalum.
i) Huruhusiwi kwenda bwenini wakati wa vipindi pasipo kibali maalum.
j) Huruhusiwi kutoka nje ya shule bila kibali kinachoonyesha unapokwenda na mda wa kurudi.
k) Huruhusiwi kutumia vifaa vya umeme bwenini au darasani, mfano Heater, Pasi nk..
l) Unapaswa kupanga mstari wakati wa kupokea huduma ya chakula jikoni.
m) Kuzingatia usafi mabwenini kila siku
n) Kuepuka kutumia lugha ya matusi kwa mtu yeyote.

MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au mtu yeyote.
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
vii. Kufuga ndevu.
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
ix. Uvutaji wa sigara.
x. Uasherati,uhusiano wa jinsi moja,kuoa au kuolewa.
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xv. Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

Imetolewa na Ofisi ya Malezi na Nidhamu.

……

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.

SHULE YA SEKONDARI LWANGWA

FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI.

SEHEMU A:

1. Jina la mwanafunzi……..
2. Mwaka wa kuzaliwa…….. kabila……..
3. Jina la mzazi/mlezi……
4. Uhusiano……..kazi yake……..
5. Anuani ya mzazi / mlezi……au namba ya simu……..
6. Mahali anapoishi mwanafunzi……..
   Umbali kuja shuleni ni km……..

Majina ya ndugu/ mlezi mwingine wa karibu:-

NO	JINA	UHUSIANO	NAMBA YA SIMU
1			
2			
3			
4			

7. Mengineyo……..(kama ugonjwa, yatima, mlemavu)

SEHEMU B. TAMKO LA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LWANGWA.

Mimi……..nimezisoma na kuzielewa sheria, kanuni na taratibu za shule na kwamba niko tayari/ siko tayari kuzifuata na kwamba sitajihusisha na uchochezi au mgomo wowote katika maisha yangu yote ya shule.

Sahihi ya mwanafunzi……..tarehe……..

SEHEMU C: TAMKO/AHADI YA MZAZI/MLEZI.

Mimi…… ambaye ni mzazi wa ……ninaahidi kwamba nitatekeleza/ sitatekeleza maagizo na mahitaji yote ya shule kama nilivyoelekezwa na kwamba niko tayari/ siko tayari kushirikiana na uongozi wa shule katika suala zima la malezi na maadili mema ya mtoto wangu kitaaluma na nidhamu yake.

Sahihi ya mzazi/mlezi……tarehe……..

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A:

To the officer from……

…….. ……

…….. ……..

…….. Date……

Re:……

Please examine the above named as to his/ her physical and mental fitness for a full time secondary school studies that may also include military training the examination should include the following categories (i-vi) each category for sub- category of which will render the applicants ineligible in case of a defect:

a) Eye sight
b) Hearing
c) Limbs
d) General diseases
e) Leprosy
f) epilepsy

PART B: MEDICAL OFFICER

(To be completed by a government medical officer)

I have examined the above named and consider that he/ she is physically fit for a full time secondary school studies.

i. (a)Eye- sight
   (B) Hearing
   (c) Speech
   (d) General diseases
   (e) Leprosy
   (f) Limbs
   (g) Epilepsy
ii. Neuroses……..
iii. Other serious diseases……..

DATE…….. SIGNATURE……

STATION…….. DATE……..